WILAYA YA NASHUA KITENGO CHA ELIMU

# UWEZO WA KUHAMASHISHA KUELIMISHA
# KARIBU KWA WILAYA YA NASHUA KITENGO CHA ELIMU

## SAIDIA MTOTO WAKO AU MWANAO KUENDELEA KIELIMU



**Wilaya Ya Nashua Kitengo Cha Elimu**
**Central Office**
**141 Ledge st**
**Nashua NH 03060**
www.nashua.ed
**603 966-1000**

**Familia , Wanafunzi , Waelimishaji .....**
**Pamoja-**

**Swahili**

## KARIBU NASHUA

Ni muhimu kwa walimu na wazazi kufanya kazi pamoja wakati wa elimu ya mtoto wao. Hii habari itakusaidia kumsaidia mtoto wako au mwanao kujifunza.

## Wafanyakazi Wanao Saidia Shule.

Hawa wafanyakazi wa 4, zaidi ya hao walimu wadarasa watakuwa kwakila shule la watoto wako. Unaweza kuita qu kukutana na wanachama wowote.

- **WALIMU WA KINGEREZA** wanasaidia mtoto wako kupata kujua lugha ya Kingereza.
- **MUONGOZI WA USHAURI** anaweza kusaidia fomu za chakula cha mchana, shughuli za baada ya shule, klabu, fedha za kusaidia kuhusu matembezi pia anaweza kujibu maswali kuhusu manitaji yote ya shule.
- **MUUGUZI WA SHULE** ako tayari kusaidia kuhusu matibabu au tatizo kuhusu afya ya mtoto wako au mwanao.
- **MUUNGANISHAJI WA SHULE NA NYUMBANI atasaidia** mawasiliano, kutafsiri katika mkutano wa mzazi na mwalimu, kujaza fomu na kusaidia kwa mengineo

## TOVUTI MUHIMU

**Wilaya Ya Nashua Kitengo Cha Elimu**(www.nashua.edu) Utakuta habari zote zashule kwenye tovuti ya wilaya ya Nashua kitengo cha elimu. Hapo utapakuta mawasiliano ya mtoto wako au mwanao na shule na kuona ratiba ya tukio kwenye shule ya mtoto wako( mwanao).

**X2**(htt://x2.nashua.edu/aspen) Alama mahudhurio ya shule ya sekondari au shule yakati wanafunzi wanaweza kukagulia au kutazamwa mtandaoniX2. Unaweza kuwasiliana na shule ya mtoto wako(mwanao) ukauliza jinsi ya kuingiza maelezo. Amwalimu wakwenye shule ya mtoto wako (mwana) Anaweza kukufundisha jinsi ya kutumia X2.

**Maktaba ya umma Nashua**(www.nashualibra.org) Unaweza kuwatembelea kwa kuomba usaidizi wakazi zako za shule za kufanyia nyumbani, mapendekezo ya kusoma, shughuli zabure, kutafuta vitabu, kujifunza kingereza, ujiunge nao kwafura wakati wa kiangazi na programu ya siku ya kutoka mapema shuleni, au kusoma magazeti kutoka inchi zingine, na mengine zaidi

**Kituo Cha Kujifuza Watu Wazima** (www.nashuaalc.org) Tovuti yao inafomu za programu ya baada yashule au michezo ya watoto wakati wa kiangazi, pia wana fomu za masomo ya watu wazima kujifunza Kingereza au kusaini kwa darasa na jinsigani ya kutumia compyuta.



## KUWASILIANA NA SHULE YA MTOTO WAKO (MWANAO)

Unahimizwa kupiga simu kwa sababu ya kawaida au kutuma maelezo kwenye shule ya mtoto wako (mwanao)

### KUWASILIANA NA MWALIMU

Jambo, jina langu ni --------- jina la mtoto wangu( mwanangu) ni -------- napenda kuongea ( kuzungumza ) na mwalimu wa Kingereza.

Hello, my name is ________________. My child is_____________. I would like to speak with the ELL teacher.

~

### MTOTO NI MGONJWA (ANAUMWA)

Jambo jina langu ni -------- jina la mtoto wangu (mwanangu) ni -------- ni mgonjwa (anaumwa) leo.

Hello, my name is ____________________. My child _______________ is home sick today.

~

### MKUTANO WA MZAZI

Jambo jina langu ni -------- jina la mtoto wangu ( mwanangu ) ni --------- napenda nisaini kwa mkutano wa mzazi na mwalimu tafadhali.

Hello, my name is __________________. My child is __________________. I would like to sign up for a parent teacher conference please.

~

### MABADILIKO YA MTOTO KUTOKA SHULENI MAPEMA

Jambo jina langu ni -------- tafadhali julisha mtoto wangu (mwanangu ) ajue leo anatakiwa:
-kutembea kwa mguu nyumbani
-kuchukua basi au nitamchukua.

Hello, my name is ____________________. Please let my child, _____________, know that today she needs to:

*walk home
*take the bus or
*_________ will pick her up.

## MAENDELEO YA RIPOTI NA KADI YA RIPOTI

Walimu wanaonyesha alama za mwanafunzi kupitia ripoti kadi wakati au kipindi cha mwaka wa shule. Hiyo ripoti kadi itakuonyesha au kukujulisha jinsi mwanafunzi wako anavyo fanya au anavyo endelea wakati wa mitihani, kazi, tabiya na jinsi anavyo hudhuria shuleni.

### SHULE YA MSINGI NA SHULE YAKATI

Wanafunzi wanaleta ripot kadi nyumbani ndani ya bahasha. Wazazi wana saini nyuma ya bahasha na wanafunzi wana rudisha iyo bahasha kwa mwalimu wao.
Unaweza kukutana na mwalimu wa mtoto wako (mwanao) naye atakusaidia kuelewa ripot kadi ya mtoto wako (mwanao).

### SHULE YA SEKONDARI

Unaweza wasiliana na shule ya mtoto wako (mwanao) ili ujue jinsi ya kuingia kwenye X2(https://x2.nashua.edu/aspen) wazazi ni lazima uwaombe habari ya kuingia shuleni kwa mtoto wako (mwanao). Wazazi wanaingia kwenye X2 kwa ajili yakusoma ripoti kadi / maendelao ya ripoti mtandaoni.

Wazazi wanaweza kuomba nakala ya maendeleo ya ripoti au ripoti kadi. Unaweza pia kukutana na mwalimu wa mtoto wako (mwanao) na atakusaidia kuelea maendeleo ya ripoti ya mtoto wako (mwanao) au ripoti kadi yake.

## MKUTANO WA MZAZI NA MWALIMU

Mkutano wa mzazi ni kitu muhimu sana utakueleweshа nini mtoto wako (mwanao) anajifunza napia jinsi anavyo endelea shuleni. pia mwalimu atakueleza kazi za shule ambazo mtoto wako anatakia kuzifanya nyumbani. kwahiyo ni umuhimu sana kukutana na mwalimu ikiwezekana umuulize maswali.

### SHULE YA MSINGI NA SHULE YA KATI

Kipindi cha msimu wa folu au mwanzoni wa mwaka wa shule walimu wana kutana na wazazi na wanazugumzia kuhusu mtoto anavyo fanya au anavyo endelea shuleni. Pia unaweza kumuomba mwalimu mukutane wakati mwingine ili akujibu maswali au tatizo unazo kuhusu kujifunza kwa mtoto wako (mwanao).

### SHULE YA SEKONDARI

Kipindi cha msimu wa folo au mwanzoni wa mwaka wa shule na kuendelea kipindi cha masika, wazazi wanakutana na walimu kwa kuongelea jinsi watoto wao wanavyo endelea au kufanya kazi za shule. Napia wanastahiu kukutana tena shuleni au wanapiga simu shuleni.

## OPEN HOUSE

Hii ni nafasi au fursa yakujua jinsi mtoto wako( mwanao ) anavyo jifunza. Open house inafanyika kipindi cha msimu wa mwanzoni wa mwaka wa shule. Angalia tovuti ya shule au kalenda ya wilaya kwenye kitengo cha shule ili ujue siku na saa ya mkutano ufuatao.

## MATEMEZI YA INJE YA SHULE

Ni kawaida kwa wanafunzi kutembelea sehemu au mahali tofauti ili wapate uwezo mpya wa kujifunza. Hayo uitwa matembezi. Hayo matembezi yanauzowefu muhimu kwa wanafunzi. Hayo matembezi yanafanyika wakati kawaida wa siku za shule.

Wazazi ni lazima wasaini fomu ya kuwaruhusu. Iyo inaruhusu mtoto wako (mwanao) kwenda matembezini na darasa lake. Mara nyingine matembezi yana garimu hela au pesa. Ikiwa mzazi hawezi kupata hela au pesa unaweza kutuma ujumbe kwa mwalimu ili ajue hayo. Mwalimu atajitaidi iwezekanavyo ili amlipie mtoto wako (mwanao).

Mara nyingine wazazi wanaweza kwenda matembezini pia. Wazazi wanasaidia wanafunzi kusikiliza kwa makini na kufuata sheriya au kanuni wakati wanajifunza. Mjulishe mwalimu wa mtoto wako (mwanao) ikiwa unataka kujitolea.

## USAFIRI WA BASI YA SHULE

Shule zinatoa usafiri ikiwa mtoto wako (mwanao) anaishi maili 2 au mbali zaidi ya shule.

**WANAFUNZI WA SHULE YA MSINGI AU SHULE YA KATI**
Kitambulisho cha kupanda basi shule inakituma nyumbani kwenu kupitia sanduku la barua kabla ya kuanza mwaka wa shule.

**WANAFUNZI WA SHULE YA SEKONDARI**
Wanafunzi wanapewa kitambulisho cha kupanda basi shuleni kwao. Icho ndicho kinacho wapa ruhusa ya kupanda basi mwaka mzima.

Ukiwa na swali kuhusu usafiri piga 603 966-1055.

## MAHUDHURIO

Mara kwa mara mahudhurio ni muhimu kwa mafanikio ya elimu. Somo linajwengwa kila siku. Watoto wanapo shinda nyumbani ina athiri ujuzi wao. Wana poteza fursa ya dhana ya mazoezi, kujiunga kwenye mjadala wa darasani, kujifunza na wen zao na kukubali usaidizi wa mwalimu. Familia kwenda likizo wakati wasiku za shule inatatiza mwanafunzi nakumletea hasara shuleni. Hii inamsababisha tatizo na kumpunguzia fursa ya kujifunza. Wanafunzi wanatarajia kuhudhuria shuleni kila siku isipokua akiganjwa (akiumwa)

## TABIA YA SHULE BORA

- Huweka kalenda ya shule kwenye jokofu. Kila jumapili usiku, wana tathmini ratiba ya jumaa au yinga.

- Unaweza wasiliana na shule ya mtoto wako (mwanao) kwa kujifunza kuhusu shughuli za baada ya shule.

- Msifu mtoto wako (mwanao) kwa kazi nzuri na umuonyeshe kazi ambazo amepata alama nyingi juu ya jokofu.

- Chunga vizuri kazi ambazo ningumu kwa mtoto wako (mwanao). Uwasiliane na mwalimu wake umuulize maswali kuhusu kazi hiyo.

- Msaidie mtoto wako (mwanao) kwa kumuuliza akueleze kile anachojifunza shuleni. Kuzungumzia kilicho tokea shuleni ili ujue nguvu ya kumbukumbu ya mwanafunzi.

- Muulize mtoto wako (mwanao) kuhusu kazi za shule anazo zifanyia nyumbani. kila mara mwafunzi anakazi  za shule ambazo anatakiwa kuzifanya.

- Kila siku angalia au chunguza mfuko wa vitabu wa mtoto wako (mwanao) kuhusu habari muhimu kutoka shuleni. Msaidie mtoto wako (mwanao) kusafisha na kupanga mfuko wake wa vitabu kila jumaa au yinga.

- Tembelea maktaba ya umma (www.nashualibrary.org) pamoja kama familia; ni bure hakuna malipo. Unaweza kuazima vitabu, muvi na miziki, kwenda kwenye tovuti ya watoto, familia na hata watu wazima, pia kutumia kompyuta kwa kazi zako binafsi, kazi za shule, au kujifurahisha.

- Wanamahali patulivu au pakimya pia wanakupa mda wakutosha wakufanya kazi zako za shule na kusoma vitabu kwa mda wadakika 20 kilasiku. Watoto ambao wanaoanza kusoma wanaweza kuangalia picha na kujiambia wenyewe hadithi kuhusu picha wanazo ziona ndani ya vitabu.  Hiyo ni fomu ya kusoma mapema.

## DESTURI NA KAWAIDA ZA MAREKANI

- Unapo kutana na mtu kwa marayako ya kwanza wa marekani wana desturi ya kupeana mkono na kuutingishana kujitambulisha  mwenyewe.
- Wana mazoezi yakuangalia mtu anaye ongea usoni.
- Ni sahihi kuomba usaidizi unapo ona mtoto wako (mwanao) akisumbuka shuleni.
- Ni vema kupiga simu shuleni ikiwa mtoto wako (wanao) haendi shuleni kwa sababu ni mgonjwa.
- Ukipiga simu, kutuma ujumbe, kutuma ujumbe kupitia simu, hata kutuma barua pepe lazima wakujibu kwa mda wa masaa ishirini na ine(24).
- Lazima uonyeshe kitambulisho chako unapo mtoa mtoto wako (mwanao) mapema shuleni.

## MAKTABA YA UMMA NASHUA

Maktaba ya umma Nashua inafungua kwa wanachama wote wa jumuia ya Nashua. Maktaba iko na programu nyingi kwa watu wa lika tofauti kutoka kwa  watoto wachanga kwa vijana pia na watu wazima. Pia wana kompyuta za umma hata vitabu ambavyo vimeandikwa kwa lugha nyingine tofauti na Kingereza.Maktaba ina programu za wanafunzi wakati wako likizo ya kianganzi na kuendelea mwaka wote washule. Tunahimiza kufurahia rasilimali nzuri ya maktaba ya umma Nashua.

## KUJIFUNZA. KUKUA. KUSTAWI

Kituo cha kujifunzia watu wazima hufundisha Kingereza bila malipo kwa watu wazima. Darasa lakutana asubui au jioni. Usajili (kuandikwa) kunaitajika kituo hicho pia kina programu ya watoto, kabla au baada ya shule, kambi ya likizo, darasa la kompyuta na HISET( mitiani ya sekondari sawa na mitiani ya chuo )  kujifunza, kukua, kustawi katika ELL ( KCKWW) Kituo Cha Kujifunzia Watu Wazima.

Wageni wapya muongenzo wao ulipandwa na kuzalishwa na Jennifer A. Chantler na Dr. Debra A. St. Lawrence, walimu wa kujitolea katika wilaya ya Nashua kwenye kitengo cha shule. Tunataka tushukuru kamati ya Uhusiano wa utamaduni, Umoja mkubwa zaidi wa Nashua, Njia ya umoja ya Nashua, Jenneth Hosking kutoka maktaba ya umma Nashua, pia Lauren Osowski kutoka kituo cha kunjifunzia watu wazima pia Bodi ya shule Nashua kwa msaada wao na kwa kujitolea kutumikia jumuiya.